# STD 6 MID TERM EXAM 2019

# KISWAHILI

**Soma vifungu vifuatacho, vina nafasi 1 - 15, kwa kila nafasi. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale manne uliyopewa.**

Maria __1__ mjini __2__ pete ya dhahabu. Alikuwa msichana aliyependa vitu vya __3__. Ali __4__ asubuhi na mapema. Baada ya muda mrefu __5__ amechoka sana. __6__ kupumzika kwenye __7__ cha mvumo. Alipoketi, aliwaona nzi wengi. Alitaka __8__ ni nini kilichokuwa pale. Kumbe kulikuwa na __9__ wa mbwa. Alishikwa na __10__ karibu aanze kutapika.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. alikwenda | B. alikuenda | C. alienda | D. alinenda |
| 2. | A. kununua | B. kununuwa | C. kununa | D. kununulia |
| 3. | A. dhamana | B. thamani | C. dhamani | D. damani |
| 4. | A. damka | B. demka | C. tamka | D. demika |
| 5. | A. alikua | B. alikuwa | C. alikuua | D. amekuwa |
| 6. | A. Aliamua | B. Aliamuwa | C. Aliamsha | D. Aliamulia |
| 7. | A. kifuli | B. kufuli | C. kubuli | D. kivuli |
| 8. | A. kuchua | B. kujua | C. kujulia | D. jua |
| 9. | A. mzoga | B. mzonge | C. mshoga | D. mzigo |
| 10. | A. kisulisuli | B. kizunzi | C. matapishi | D. kichefuchefu |

Utunzaji __11__ wanyama ni __12__ la kila __13__ katika jamii. Wapo watu __14__ hawajali maslahi ya wanyama hata __15__.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 11. | A. wa | B. ya | C. la | D. za |
| 12. | A. chukumu | B. hukumu | C. jukumu | D. wazo |
| 13. | A. kimoja | B. mmoja | C. moja | D. umoja |
| 14. | A. ambaye | B. ambayo | C. ambae | D. ambao |
| 15. | A. kidogo | B. mdogo | C. wadogo | D. kamwe |

**Kutoka swali la 16 - 30, jibu swali kulingana na maagizo.**

16. Sehemu kortini kama sanduku ambamo mshtakiwa husimamia ni __________.

A. gereza B. korti
C. korokore D. kizimba

17. Dawa tuliyoinywa ni shubiri. Hii ni kumaanisha __________.

A. chungu sana B. haina tiba
C. ni kidogo D. ni ghali sana

18. Barabara ______ itakarabatiwa mwezi ujao.

A. lingine B. nyingine
C. Ingine D. zingine

19. Ni sentensi gani iliyoandikwa sahihi?

A. Miti nyingi imekatwa
B. Watu wasaba waliajiriwa
C. Nyumba nyingi zimejegwa
D. Maji ambayo imeletwa ni chafu

20. **Kamilisha sentensi hii:-**

Mtoto amekula na ameshiba.

A. Mtoto hajakula na ameshiba
B. Mtoto hajala wala hajashiba
C. Mtoto hakula na hakushiba
D. Mtoto hakukula na hakushiba

21. **Kamilisha methali hii:-**

Mti hauendi ila kwa __________.

A. nyenzo B. shoka
C. moto D. mjenzi

22. Kikembe cha nyuki ni __________.

A. buu B. kiyoyo
C. kimatu D. jana

23. Wasichana ________ huvalia ________.

A. wasafi, nadhifu
B. safi, nadifu
C. safi, nadhifu
D. wasafi, wanadhifu

24. **Tegua kitendawili hiki:-**

Mama lazima afe, ndipo mtoto wake azaliwe hai.

A. siafu B. mbegu
C. buibui D. ng'ombe

25. Wanafunzi wote walinyeshewa walipokuwa wakienda nyumbani wakaloa __________.

A. chopi B. chepechepe
C. kochokocho D. chubwi

26. Kitenzi fuma katika hali ya kutenda ni ______.

A. fumua B. fumuka
C. fumia D. fumiwa

27. Nomino mitume hapatikani katika ngeli ipi?

A. U - I B. U - ZI
C. I - I D. A - WA

28. Mtu mwenye nundu mgongoni huitwa ______.

A. kibogoyo B. kibyongo
C. kiguru D. kigongo

29. Ni neno lipi si nomino kati ya maneno haya?

A. Kochi B. Soma
C. Punda D. Upepo

30. **Andika wingi wa sentensi hii:-**

Unga ulioletwa ni mweupe.

A. Unga zilizoletwa ni nyeupe
B. Nyunga zilizoletwa ni nyeupe
C. Unga ulioletwa ni mweupe
D. Unga iliyoletwa ni nyeupe

**Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 31 - 40.**

Kalasi aliishi katika uchochole mwingi baada ya kuwa yatima. Watu wengi waliweza kumjua kwa sababu ya wema wake. Alikuwa mtiifu na mzuri kwa kila mtu aliyemkuta. Ama kweli tabia ni ngozi. Tabia ya Kalasi haikubadilika hata baada ya vifo vya wazazi wake.

Mzee mmoja aliyekula chumvi nyingi alimsihi Kalasi amchungie mbuzi wake. Mzee huyo hakuwa na jamaa hata mmoja ambaye angemsaidia kupeleka mbuzi hao malishoni. Kalasi alikubali na kila wakati aliwatunza mbuzi hao malishoni kama wake.

Baada ya miezi mitatu, mzee huyo alianza kuugua na akawa katika hali mahututi. Alianza kuchungulia kaburi. Alitamani aendelee kuishi ili amtunze Kalasi kama mwanawe. Siku zake za kuishi zilielekea kuisha. Aliwaza na kuwazua jinsi ya kunsaidia Kalasi kwa wema wake. Asubuhi moja alimwita na kumjulisha kuwa amemwachia mbuzi wake wote kuwa mali yake. Baada ya kumaliza maneno hayo, alikata roho. Chambilecho wahenga, wema huzaa wema.

**31.** Ni methali ngapi zimetajwa katika habari hii?

A. 2 B. 1

C. 4 D. 3

**32.** Kalasi alikuwa na tabia ya aina gani?

A. Ukorofi B. Ukaidi

C. Utiifu D. Uchovu

**33.** Aliyekula chumvi nyingi, maana yake ni ____________.

A. kulamba chumvi

B. kuishi mbali

C. kukolea kwa chakula

D. kuishi miaka mingi

**34.** Kwa nini mzee huyo alimsihi amchungie mbuzi?

A. Kalasi ni mwanawe

B. Hakuwa na jamaa wa kusaidia kuchunga mbuzi

C. Alikuwa amemwajiri Kalasi

D. Kalasi alikuwa akirandaranda mtaani

**35.** Kuwa katika hali mahututi ina maana gani?

A. Kuugua sana

B. Kuzeeka sana

C. Kutajirika mara tatu

**36.** Kuchungulia kaburi ni ____________.

A. methali B. semi

C. istiara D. kitendawili

**37.** Utajiri wa Kalasi ulitokana na ____________.

A. kiburi chake B. majivuno yake

C. wema wake D. utanashati wake

**38.** Mali yanayoachwa na marehemu kwa mtu mwingine huitwa ____________.

A. mirathi B. tuzo

C. mahari D. ada

**39.** Kulingana na ufahamu huu, mzee mwenye mbuzi aliaga dunia kwa sababu ________.

A. ya uzee uliokithiri

B. ya kupeleka mbuzi malishoni kila siku

C. ya kuwaza na kuwazua sana

D. ya uzee pamoja na maradhi

**40.** Wema huzaa wema, ina maana kuwa ______.

A. tunapotendea wengine wema, nasi tutatendewa wema wakati mwingine

B. lazima utendewe wema hata usipotenda mema

C. malipo ya wema ni mbuzi

D. tungojee tutendewe mema ili tutende mema

**Soma shairi hili kisha ujibu maswali 41 - 50.**

Natunga wangu utunzi, vina napanga imara
Nyie mlio wapenzi, kiini ni mazingira
Vivyo tulani simanzi, kwa chanzo cha afya bora
Je, ni vipi mazingira, kwa afya ya binadamu?

Nasikitika kwa majonzi, takataka kila mara
Maji machafu na vitunzi, huharibu ustara
Uvundo huleta inzi, inzi heleta kolera
Je, ni vipi mazingira, kwa afya ya binadamu?

Hata nyinyi wanafunzi, usafi kwenu ni bora
Mnaposoma vitenzi, vile vile misafara
Viwanda na yenu jinsi, ni hatia kwa wizara
Je, ni vipi mazingira, kwa afya ya binadamu?

41. Shairi hili lina beti ngapi?
   A. Tatu
   B. Nne
   C. Tano
   D. Kumi na sita

42. Vina vya kati na vya mwisho ni __________.
   A. ra, mu   B. ra, nzi
   C. nzi, ra   D. mu, ra

43. Ubeti wa kwanza mshororo wa nne una mizani mingapi?
   A. 4   B. 8
   C. 15   D. 16

44. Kibwagizo cha shairi hili ni _________.
   A. Tamati haki kitanzi, ufate niliyochora
   B. Je, ni vipi mazingira, kwa afya ya binadamu?
   C. Nasikitika kwa majonzi, takataka kila mara
   D. Natunga wangu utunzi, vina napanga imara

45. Shairi hili ni la aina gani?
   A. Takhmisa
   B. Tarbia
   C. Tathlitha
   D. Tasdisa

46. Stadi anayetunga na kuimba mashairi huitwa?
   A. Malenga
   B. Manju
   C. Sogoro
   D. Mutribu

47. Ni ujumbe upi tunaopata kutoka kwenye shairi hili?
   A. Tule kitanzi kwa sababu ya mazingira yetu
   B. Tusinadhifishe mazingira yetu
   C. Tuyapuuze mazingira yetu
   D. Tuhifadhi mazingira yetu

48. Jina la bandia analojipa mshairi huitwa __________.
   A. malenga
   B. lakabu
   C. kungwi
   D. somo

49. Shairi hili lina vipande vingapi katika kila mshororo?
   A. Vinne
   B. Vitatu
   C. Viwili
   D. Kumi na sita

50. Kichwa kifaacho shairi hili ni ___________.
   A. uchafu
   B. mazingira
   C. usafi
   D. takataka